# KISWAHILI PP 3 KEY LIGHT MOCK

## 2023 KCSE EYE SIGHT

TOPLIGHT PUBLISHERS KENYA PANEL WORK
CONTACT US 0729125181
0729125181
abrahammariera@gmail.com

FOR MARKING SCHEME AND MORE CALL SIR ABRAHAM **0729125181**

JINA ……………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA…………………

SHULE……………………………………..……. SAHIHI………...……………………..

TAREHE…………………..……………LENGO…………………………………………

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**

**FASIHI**

**Term 2 2023**
**MUDA: SAA 2 ½**

**SERIES 1 2023 KCSE MOCK**

**MAAGIZO:**

a) Jibu maswali manne pekee
b) Swali la kwanza ni la **lazima**
c) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**SEHEMU YA A: USHAIRI**

**Swali la Lazima**

**1.** ***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata:***

**Shimo: Ali Salim Zakwany**

1. Mwambieni kibushuti, asiruke shimo lile
   Kimo chake kama goti, kwenda ng'ambu sifikile
   Mtu haoli bahati, akasahau umbile
   Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

2. Afanyayo ni hatari, sijitie mpulele
   Mambo yote ajasiri, shari asithibutile
   Mjalia watu kheri, shairi ni yake vivile
   Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

3. Asambe ndiyo busara, kutenda kitendo kile
   Itamuwia hasara, na madhara kama yale
   Mola mwingi wa subira, ajapo chomwa vidole
   Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

4. Licha na yeye nyadungo, chuya katika mchele
   Hata warefu ja pondo, hawatusi shimo lile
   Walojaribu kitendo, shimoni watumbukile
   Kila muwania mbele, na nyuma sisahawile

5. Nimefika kituoni, nasema mumuwasile
   Mfua maji ngamani, ili kwamba sizamile
   Chombo huungia mwambani, na nahodha ni yuyule
   Kila muwania mbele, na nyuma 'sisahawile

**Maswali**

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)
b) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 4)
c) Taja na utoe mifano ya tamathali za usemi mbili zinazopatikana katika shairi. (alama 4)
d) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
e) Kwa kutoa mifano minne, eleza aina moja ya idhini ya kishairi iliyotumika zaidi katika shairi. (alama 3)
f) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari. (alama 4)

**SEHEMU YA B: RIWAYA – CHOZI LA HERI (ASSUMPTA MATEI)**

2. "Jua linalochomoza halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua..... Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua..."

   (i) Eleza aina za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 8)
   (ii) Eleza mbinu nyingine ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
   (iii) Eleza sifa na umuhimu wa msimulizi wa dondoo hili. (alama 10)

3. Lakini itakuwaje 'historical injustice' nawe Ridhaa hapo ulipo sicho kitovu?
   (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (ii) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
   (iii) Eleza sifa nne za mzungumzaji wa maneno haya. (alama 8)
   (iv) Eleza mambo matatu yaliyowakumba walioishi penye kitovu kisicho chao. (alama 6)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA - BEMBEA YA MAISHA (Timothy Arege)**

4. Ukirejelea Anwani ya Tamthilia ya Bembea ya Maisha, onyesha namna wahusika wanavyobembea maishani mwao. (alama 20)

5. Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kuwa mchezo kumbe ilikuwa kweli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silezi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. Siku hazigandi wala jana hairudi. Sasa jana imebaki kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika."

   a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake (alama 4)
   b) Eleza kwa mfano mbinu nne za kimtindo zilizotumika (alama 4)
   c) Barusha toni katika dondoo hili. (alama 2)
   d) Ni maudhui gani yanayojitokeza katika dondoo hili? (alama 4)
   e) Onyesha sifa za mzungumzaji zinazodhihirisha kuwa silezi zao hawakuzila kwa furaha. (alama 6)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI - MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI ZINGINE.**

6. (a) Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo lifuatalo. (alama 6)

"Jimbo la matopeni lilikuwa limegeuzwa ngome ya watu fulani binafsi. Watu wenye ushawishi mkubwa serikalini! Watu wasiojali maisha ya wapiga kura kama Machoka na Zuhura. Wapiga kura walioamka siku hiyo asubuhi ya majogoo, wakastahimili baridi kali ya bukrata. Wakavumilia jua kali la mchana. Zuhura alikumbuka namna yeye na wenzake walivyotunga foleni ndefu kwenye vituo vya kupigia kura. Yote haya wakiwa na matumaini ya maisha bora ya baadaye, si bora maisha! Kumbe wajinga ndio waliwao! Mzigo mzito wa maisha haukuwatisha wala kuwakosesha usingizi viongozi wao. Ama kweli, mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi. "

(b) Onyesha namna wanamatopeni wanavyokumbwa na madhila kwa kurejelea hadithi ya "Msiba wa kujitakia" (alama 14)

7. "Katika hali ile ya uchungu, kilio na mtanziko wa mawazo, akaiona simu yake imeanguka chini ya kitanda….. Haidhuru hata kama atamuunga mkono mwanawe."
   (i) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   (ii) Fafanua mbinu ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
   (iii) Eleza sifa nne za anayerejelewa katika dondoo hili. (alama 4)
   (iv) Eleza jinsi "taasubi ya kiume" inavyoshughulikiwa na mwandishi wa "fadhila za punda". (alama 10)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

8. Ewe Mainga wa Ndumi
Siwe uloambia akina mama
Siku tulopiga foleni
Chakula cha msaada kupata
Turudishe vifaranga kwenye miji
Wageuke vijusi tena
Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita
Matusi ukitema

Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?
Uhitaji wetu ukatutuma
Kuokota vihela uloturushia
Ukatununua, kura ukapata?
Sasa miaka mitano imetimia
Waja tulaghai tena
Mainga wa Ndumi huna lolote safari hii
Ubunge umekudondoka ukitazama
Wanyonge tumeamua
Kwingine kujaribu.

a) Eleza aina ya kipera hiki. (alama 2)
b) Huku ukitoa mifano, tambua mbinu za lugha nne zilizotumiwa katika utungo huu. (alama 8)
c) Tambua nafsineni katika utungo huu. (alama 2)
d) Fafanua toni ya utengo huu. (alama 2)
e) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. (alama 6)

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………….

........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
.....................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................
........................................................................................................................

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM **0729125181**

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM 0729125181

.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................
.............................................................................................................

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM **0729125181**

# KISWAHILI PP3

JINA …………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA………………….

SHULE………………………………….……. SAHIHI………..……………………..

TAREHE…………………..……………LENGO…………………………………………….

SAA:2.30 MIN **SERIES 2 KCSE MOCK**

**SERIES 2 MOCK**

**MAAGIZO**

- g) Jibu maswali manne pekee.
- h) Swali la kwanza ni la lazima.
- i) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; tamthilia, riwaya, hadithi fupi na fasihi simulizi.
- j) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- k) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- l) Majibu yote sharti yaandikwe kwa kijitabu cha majibu ulichopewa.
- m) Andika nambari ya maswali uliyoyajibu.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**SEHEMU YA A: USHAIRI**
**SWALI LA LAZIMA**

**MBELE YA SAFARI**

(v) Ilipoanza safari , ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

(vi) Njaa ikawa dhabiti ,na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti ,dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

(vii) Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari,utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari , juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

(viii) Ile ilikuwa ndoto , mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto,sahala ‘mekuwa dhiki
Wagombanio kipato,utashi haukatiki
Nakutabakari

(ix) Msafara ukasita , kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita , mlima haupandiki
Basi sote ‘kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

(x) Tukiwa migongo wazi ,tukainama kwa shaki
Tukawa’chia ukwezi , kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi ,Kuteremsha miliki
Wakaitapia

(xi) Wakafikia makazi,ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

(xii) Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema , kwa umati halaiki
Imezima nia yote ,kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

f) Eleza safari inayolejelewa katika shairi hili. (al 2)

g) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. (al 6)

h) Taja na ueleze bahari mbili za shairi ukizingatia : (al 4)

9. Mizani ;

10. Vina

i) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (al 4)

j) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita. (al 4)

k) Eleza umbo/ muundo wa shairi hili. (ala 2)

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**
**Timothy Arege**
**BEMBEA YA MAISHA**

2. Hiyo ndio ajabu! Kizazi hili hakitaki kufanya kazi. Kinataka kuja kazini kwa sababu ya mshahara tu. Wachapa kazi hodari ni njozi iliyopotea.

7. Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala 4)
8. Eleza sifa za msemaji wa dondoo hili. (ala 4)
9. Fafanua imuhimu wa msemewa katika kazi ya Bembea ya Maisha. (ala 4)
10. Taja na uonyeshe mbinu za uandishi zilizotumika katika dondoo. (ala 4)
11. Eleza maudhui yanayokuzwa katika muktadha wa dondoo. (ala 4)

3. Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. (ala 20)

**SEHEMU YA C: Riwaya**
**Assumpta Matei**
**Riwaya ya Chozi la Heri**
**Jibu swali la 4 au 5**

4. "Siku moja nitakuwa mtetezi wa haki za kibinadamu, hususan haki za watoto."

(iv) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
(v) Jadili sifa tano za mzungimzaji. (ala 5)
(vi) Kwa kutumia hoja kumi na moja . Onyesha jinsi jamii ya wahafidhina inavyokiuka haki za watoto. (al 11)

**Au**

5. Onyesha jinsi maudhui ya usaliti yanavyojitokeza katika riwaya ya Chozi la Heri. (al 20)

**HADITHI FUPI**
**D.W Lutomia na Phibbian Muthama: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine***
**Jibu swali la 6 au la 7**
6. "Isije ikawa mwenye nyumba kuja na yeye mpangaji akachelewa kumfungulia mlango; itakuwa balaa bin beluwa"

6. Eleza muktadha wa dondoo hili (ala 4)
***7.*** Jadili umuhimu wa mwenye nyumba anayerejelea (ala 6)
***8.*** Maisha yalikuwa balaa bin beluwa kwa mpangaji. Thibitisha ( ala 10)

***7.***
***(a)*** Machoka alikumbuka kauli ya jirani yake, Zuhura, aliyeishi kumkumbusha, "wetu ni wetu, hata akiwa mbaya … wetu. Hatuna budi ila kumchagua yeye. Lisilobudi hubidi. Awe amesoma ama hajasoma, angali wetu."leo hii hata Zuhura mwenyewe alikuwa anajutia kumchagua huyo wetu.
Kwa muda mrefu, Machoka na Zuhura walikuwa kama fahali wawili hawakai katika zizi moja. Kisa na maana, ni wafuasi wa watu wawili tofauti. Leo hii kinachowaleta pamoja Machoka na Zuhura ni udhikinifu, hali ngumu ya maisha, mfumuko wa bei za bidhaa muhimu na kutozwa ushuru wa kiwango cha juu na serikali hiyo hiyo ya 'watu wao'. Zuhura alisuta nafsi yake. Alikuwa akiitazamia nchi nzuri na maisha bora baada ya uchaguzi. Alitazamia 'watu wake' wangezitimiza ahadi walizozitoa wakati wa kampeni zao. Leo hii imebakia kujuta. Kujuta ghya ya kujuta! Tayari alikuwa amekwishafanya kosa. Kosa ambalo alifahamu lilikuwa la kujitakia. Ulikuwa mwiba wa kujidunga usiokuwa na kilio wala kuambiwa pole. Maji yalikuwa yashamwagika, katu hayangeweza kuzoleka…"
Chambua maudhui katika dondoo hili. (ala 12)

(b) Eleza sababu nne zinazochangia jimbo la Matopeni kutoshuhudia maendeleo ya kisiasa tangu nchi kupata uhuru . (ala 8)

**SEHEMU YA E**
**FASIHI SIMULIZI**
8. i)Eleza maana ya misimu. (al 2)

ii)Taja mambo manne ya kimsingi yanayochangia kuchipuka kwa msimu. (al 4)

iii)Eleza umuhimu wa misimu katika jamii. (al 10

iv)Taja sifa nne za misimu. (al 4)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………………

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM **0729125181**

**JINA …………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA………………….**

**SHULE………………………………….……. SAHIHI………..……………………..**

**TAREHE…………………...……………LENGO………………………………………….**

**MUDA SAA 2HR$30 MIN**

# Maagizo

**SERIES 3KCSE MOCK**

9. *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
10. *Jibu maswali **manne** pekee.*
11. *Sehemu zote ni **lazima**.*
12. *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
13. *Karatasi hii ina kurasa **14**. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*
14. *Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| JUMLA | 80 | |

**SEHEMU A: USHAIRI**

**1.** *Soma shairi hili kisha ujibu maswali.*

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali
Ubavuni umuweke, umtowe kule mbali
Maskanini afike, umtindie fahali
Utamu anufaike, sima, bada au wali
Hatimaye ateuke, kwa viliwa vya samli
*Mwanadamu simuamini, afadhali nyama lumbwi*.

Mwanadamu umjenge, awe mwenye kutajika
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka
Nao mkono umuunge, vyake viwe vyaungika
Dhorubani umkinge, asipate kudhurika Mara
atakusahau, wema wako kafukia.

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie
Amani yako umpeo, fanaka uirajue
Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue
Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue
Ndio wake mwelekeo, yuauma avuvie
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame.

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililo jema
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema
Viteko siwe akali, kumbizo zikaterema
Binadamu takudhili, dhili zako kuzitema
Licha ya zote jamili, mwanadmu si muema Mwanadamu
ni mtu, lakini nusu mnyama

f) Onyesha kinaya cha mwanadamu anayezungumziwa. (alama 4)

g) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)

h) Taja na ueleze bahari **nne** za shairi hili. (alama 4)

i) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

j) Onyesha mbinu **nne** alizotumia malenga ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi

katika shairi hili. (alama 4)

f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 4)

**SEHEMU B: FASIHI SIMULIZI**

**2.** *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali*

Angole angole mwanangu
Mwanangu nakuchombeza
Nakuchombeza ulale
Ulale ukiamka
Nikupikie ubwabwa
Na mchuzi wa papa
Ukilia waniliza, wanikumbusha
Ukiwa wa baba na mama

Baba na mama watende
Ilimu kunikatizia
Ng'ombe, mbuzi kupokea
Kunioza dumu kongwe
Haliuki na halende
Kazi kupiga matonge

Likingia mvunguni
Lavunjavunja vikombe
Likilala kitandani
Languruma kama gombe

l) Bainisha kipera cha utungo huu. Thibitisha. (alama 2)

m) Eleza ujumbe unaofumbwa katika wimbo huu. (alama 5)

n) Tambua mbinu za kifani ambazo zimetumiwa kuwasilisha utungo huu. (alama 3)

o) Bainisha shughuli **mojamoja** ya kijamii na ya kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. (alama 2)

p) Unakusudia kukusanya data kuhusu kipera hiki. Eleza manufaa **manne** ya kutumia mahojiano. (alama 4)

q) Kipera hiki kinazidi kufifia katika jamii yako. Fafanua njia **nne** ambazo jamii ya kisasa inaweza kutumia kukuza na kuendeleza kipera hiki. (alama 4)

**SEHEMU C: RIWAYA**

**Assumpta K. Matei: Chozi la heri**

**Jibu swali la 3 au 4**

**3.** "Hili ni wingu la kupita na bila shaka wingu la kupita halipaswi kumtia mkulima matumaini. Tutapambana, sheria tunaijua."

(xiii) Bainisha mitindo **sita** inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 6)

(xiv) Bainisha mazaji inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(xv) Kwa hoja **kumi na mbili,** onyesha namna jamii ya *Chozi la Heri* ni mfano wa jamii iliokosa ukomavu wa kisiasa. (alama 12)

**4.** "Yote haya yamewezekana kutokana na mwongozo mlionipa nyinyi. Zaidi, utulivu nilioupata nilipoambulia familia hii ulinipa msukumo kila mara nilipokabiliwa na ndaro."

12. Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
13. Eleza mchango wa mzungumzaji wa maneno haya katika kukuza ploti ya riwaya ya *Chozi la Heri*. (alama 5)
14. "Familia ndicho kitovu cha ufanisi wa mtoto maishani." Thibitisha kwa mujibu wa riwaya ya *Chozi la Heri*. (alama 11)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

*D. W. Lutomia na Phibiana Muthama: Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 5 au 6*

**5.**

*Nipe Nafasi – Mzamane Nhlapo*

(v) Eleza tafsiri mbalimbali za kichwa cha hadithi hii, '*Nipe Nafasi*' (alama 7)

*Pupa (F. M. Kagwa)*

(vi) Fafanua umuhimu wa mandhari ya *Chenga-ways* katika kujenga hadithi *Pupa*. (alama 5)

*Toba ya Kalia (Douglas Ogutu)*

(vii) "Ni kutokana na mchango wako kupitia *twitter* na *facebook* katika maswala mbalimbali ambapo iliamuliwa upewe fursa ya kuzungumza moja kwa moja na watazamaji wetu."

Eleza nafasi ya vijana kwa mujibu wa hadithi *Toba ya Kalia*. (alama 8)

**6.**

*Nilitamani* (*Phibiana Muthama)*

11. "Wakati anaongea kwa simu, nikawa najifungua mkanda. Nikafaulu. Nikajaribu kufungua mlango. Duh! Ulikuwa ushatiwa *loki*. Sijui nilipata wapi nguvu za kupitia juu yake! Nikaponyoka pyu! Nikakimbia mguu niponye. Nilikimbia nisijue niendako. Nikakimbia. Sitaki kuangalia nyuma kwa kushtukia yaliyonikuta. Nilikata katikati ya misitu sijui nielekeako ila mbali na Romeo na pepo yake. Nimekaza mwendo huku nahema, pumzi si zangu! "

a. Fafanua aina za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 5)

b. "Tamaa mbele mauti nyuma." Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi: *Nilitamani*. (alama 7)

*Kifo cha Suluhu – Dominic Maina Oigo*

12. "Aliyaacha machozi yamtoke shibe yake kwani asingeweza kujizuia. <u>Barua ile</u> <u>ilimfichulia siri si haba</u>"

Thibitisha kauli iliyopigwa mstari ukirejelea hadithi *Kifo cha Suluhu*. (alama 8)

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM **0729125181**

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM **0729125181**

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM **0729125181**

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM **0729125181**

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

**JINA …………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA…………………**

**SHULE………………………………….……SAHIHI…….……..……………………..**

**TAREHE…………………..……………LENGO……………..……………………………**

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**

# SERIES 4 2023 KCSE MOCK

## KIDATO CHA NNE

**MUDA: SAA 2 ½**

***MAAGIZO:***

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali **manne** pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la **lazima.**
e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
f) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
g) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
h) Karatasi hii ina kurasa **7** zilizopigwa chapwa
i) Watahiniwa ni **lazima** wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

***KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.***

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |
| | | |

**SEHEMU A: SWALI LA LAZIMA**

**(ALAMA 20)**

**1. USHAIRI**

**UTU NI NINI?**

Utu na ubinadamu, ni kama yai na kuku

Utu ni ile nidhamu, *mola aliyokhuluku*,

Ubinadamu ni damu, ya utu wa kila siku,

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Ye yote mwanaadamu, ana asili ya utu,

Ya'ni kwenye yake damu, hakikosi hiki kitu,

Utu sifa maalumu, ya mtu kuitwa mtu,

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu ni kiumbe hai, tunacho chaonekana

Utu kamwe haudai, tabia ya kujivuna,

Utu ni ule uhai, ushikao uungwana,

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu huweza pimika, kwa hisia ya akili,

Huweza kuhifadhika, kulingana na *fadhili*,

*Utu huweza pendeka, palipo na maadili*

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu unayo aibu, na *tabia ya muhali*,

Utu huenda na jibu, la Imani na ukweli,

Utu huiona tabu, tabia ya ujahili,

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Filosofia ya utu, inapinga ubinafsi,

Utu hautaki kitu, cha upeke wa nafsi,

Utu hauna kiatu, cheupe au cheusi,

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu wa kweli kwa *mja*, ni wenzake kuwajali,

Utu huiona haja, ya kujua watu hali,

Utu ni kuwa pamoja, kwenye shida mbalimbali,

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu ni ubinaadamu, udugu na wenzi wako,

Utu wote waheshimu, kwa nidhamu na kicheko,

Utu ona mwanadamu, sijitenge peke yako,

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Ingawaje tu dhaifu, katika ubinafsi,

Utu kweli nausifu, ubinadamu halisi,

Utu ni sifa tukufu, iletayo kila *nemsi*,

Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

a) Tambua aina  ya shairi hii kwa kutolea ithibati.
(alama 2)

b) Taja sifa tano za mtu mwenye utu kulingana na shairi.
( alama 5)

c) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa na mshairi.
(alama 2)

d) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo.
(alama 3)

i) vipande

ii) vina

iii) mpangilio wa maneno

e) Tambua nafsineni katika shairi.
(alama 1)

f) Tambua mbinu tatu alizotumia mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi.
(alama 3)

g) Andika ubeti wa saba kwa lugha nathari.
(alama 4)

**SEHEMU B: RIWAYA,**

**A Matei: Chozi la Heri**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. Jadili mchango wa wazazi na walezi katika kusambaratisha familia katika riwaya ya Chozi la Heri
(alama 20)

***au***

3 Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua...Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; matone yanayoanguka kwenye ngozi laini zą wanangu wakembe... ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu... Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu.... Siye, siye, siye-e-e-e. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha kikwi... Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira!

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
b) Jadili aina ***nne*** za taswira katika dondoo hili
(alama 4)
c)Bainisha vipengele vingine **vinne** vya kimtindo katika dondoo hili
(alama 4)
d) Bainisha toni ya dondoo hili.
(alama 2)
e) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili
(alama 6)

## SEHEMU C. TAMTHILIA

**T. Arege: Bembea ya Maisha**

**Jibu swali la 4 au la 5**

4."... wakati mwingine mwindaji huwa mwindwa. Hata kijijini wanaishi watu . Watu hao hawakumbwi na dhiki kiasi hiki. Ya nini kung'ang'ana kuyatafuta maisha kama kwamba hayapiti? Maisha ni mshumaa uso mkesha! Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuuzima kabla ya kulika hadi nchani.”

**Maswali**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama. 4)

b) Bainisha toni katika kauli hili
(alama. 2)

c) Eleza vipengele **<u>vinne</u>** vya kimtindo alivyotumia msemaji kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe.
(alama. 4)

d) Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza ploti ya tamthilia hii.
(alama 10)

***au***

5. (a) Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya Luka, Beni na Yona katika kujenga tamthilia ya “Bembea ya Maisha”
(alama 10)

(b) "Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa michezo.Huungwa na mchezo kuanza tena." Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutolea mifano mwafaka tamthiliani.
(alama. 10)

**SEHEMU YA D**

**Hadithi Fupi – Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine – Dw Lutomia**

***Jibu swali la 6 au la 7***

***Kifo cha Suluhu***

6. Mume wangu, hebu zivute fikra zako miaka kumi na mitano iliyopita tulipoingia katika mkataba wa ndoa. Kwa nini unataka kujitia hamnazo kuhusu ahadi ulizozitoa? Umesahau namna tulivyohangaika, tukachekwa na watu, tukakosa hata marafiki na hatimaye tukabandikwa majina ya ajabu? Umesahau, mume wangu? Umesahau namna kazi yako ya kuuza makaa ilivyofika hatima ya ghafla baada ya serikali kupiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la Dafrao? Naomba ukumbuke. Ninaamini huenda umesahau! Ama cheo chako cha ubunge ulichokipata kwa mbinu nizijuazo mimi kimekulevya na kukufanya uisahau familia yako?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 5)

b) Fafanua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili.
(alama 6)

c) Tambua toni iliyotumika katika dondoo hili.
(alama 2)

d) Fafanua umuhimu wa ujumbe alitoa mnenaji wa maneno haya. Tumia hoja nane.
(alama 8)

**au**

7. "**Wewe mke sampuli gani usiyetaka kumuunga mkono mmeo?"**

Kwa kurejelea hadithi hii na nyingine zifuatazo, jadili changamoto anazopitia mnenewa pamoja na wahusika wa jinsia yake.
(alama 20)

***Ahadi ni deni.***

***Hadithi ya Nipe nafasi***

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

Hapo zamani za kale, Nyani na Mamba walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Watoto wao walipendana na kufaana kama ndugu wa toka nitoke. Familia ya Mamba aliishi mtoni nayo ya Nyani aliishi katika msitu uliokuwa maili thelathini kutoka mtoni. Kila mara marafiki hawa walitembeleana na kusaidiana kwa hali na mali. Kwa vile Mamba alikuwa mvuvi msahuhuri, aliweza kumwauni Nyani na aila yake kwa samaki wa aina mbalimbali. Nyani naye alimpelekea Mamba matunda na nafaka kutoka shambani mwake.
Urafiki wao ulikita mizizi na kunawiri Zaidi wakati Mamba alipokuja kwa Nyani kumposea mwanawe binti. Ukwe uliutilia viungo uhusiano wa Nyani na Mamba wakawa wanagandana kama kupe na mkia wa Ng'ombe. Wakatenda mengi pamoja. Wakazungumza ya kupwa na ya

kujaa. Hakuna hata mmoja wao aliyeutilia shaka uaminifu wa mwenzake. Wake zao nao walifuata kaida ya maji kufuata mkondo. Walikuwa masahibu wa chanda na pete.

Msimu mmoja wa mapukutiko ulishuhudia mabadiliko ya kudumu katika maisha ya Nyani na Mamba. Wakati huo, bahari ilichafuka si haba. Kazi ya Mamba ya uvuvi ikaanza kukabiliwa na majabali ya kila aina. Kila mara Mamba alipokwenda uvuvini, alirudi akichekelewa na nyavu zake. Hakuambulia chochote. Njaa ilianza kubisha hodi katika familia ya Mamba. Hali hii ilitishia kuutia ufa urafiki kati ya Mamba na Nyani. Mamba alivamiwa na pepo ambaye hata yeye alishindwa kumfahamu. Kila mara alipomwona. Nyani au watoto wake alitamani kumdakia na kumla mzima mzima. Kadiri aalivyojaribu kujiasa dhidi ya fikira hii mbovu ndivyo moyo wake ulivyoendelea kumshauri, “Una njaa bwana, familia yako itaangamia. Je huoni rafiki yako na familia yake wanaweza kuwa kitoweo? Utaendelea kula wishwa hadi lini? Mbona huyo Nyani ambaye anajiita rafiki yako sasa amekata guu humu? Mbona haji tena kukutazama? Hata karafuu alizokuwa akikuletea ameacha kuleta. “Mamba akaanza kumshuku rafiki yake na akasadiki kuwa Nyani alikuwa mla naye tu.

Usiku mmoja baada ya kula mate na kujilaza kitandani mwake akihesabu nyota, wazo lilimjia. Alikata shauri kumlaghai rafiki yake wa miaka mingi ilia pate kujiokoa yeye na familia yake kutoka katika kinamasi cha njaa. Asubuhi yake alikwenda kwa Nyani akiwa amejinamia kwa jitimai. Alisema, “Rafiki yangu, jana tulipoagana nilipata tanzia. Mjumbe kutoka kijijini aliniarifu kuwa baba yangu ni mgonjwa mahututi. Alisema kwamba baba ananitaka nyumbani upesi,” Habari hizi zilimtia Nyani majonzi makuu. Alimwahidi Mamba kwamba wangeandamana pamoja. Kwa vile Nyani hangeweza kutembea majini, ilibidi abebwe na Mamba. Alipatwa na kichefuchefu na manyezi kila alipotazama bahari iliyojitandaza mbele yao kwa mbwembwe. Hata hivyo, Mamba alimhakikishia kuwa wangefika salama. Naye kwa Imani iliyotokana na urafiki na mazoea ya miaka mingi, alitulia.

Safari ilikuwa ndefu na yenye machovu yaliyomfanya Nyani kulala mgongoni mwa Mamba. Walipofika kwenye vina vya maji, Mamba aliamua kumpasulia mbarika Nyani. “Rafiki yangu, nimekuwa nikidhani wewe ni rafiki wa dhati, kumbe uzuri wako wa mkakasi? Mimi na wanangu tumetafunwa na njaa kwa miezi kadha sasa huku maghala yako yakishiba na kutapika chakula. Hujadiriki hata siku moja kuja kujua kama nimepata hata senti moja ya kusagia mkunguni. Jana usiku nilipokuwa nikiwazia hali yangu, nilioteshwa katika ndoto kwamba kama ningepata moyo

wako na kuula, basi hali ya uhitaji ingeniishia. Moyo wangu unaniuma sana kukufanyia tendo hili, hata hivyo lisilo budi hutendwa."

Nyani alipigwa na butwaa nusura moyo wenyewe ujikabidhi kwa Mamba. Hata hivyo, akili yake nyepesi ilifanya kazi. Alimwambia Mamba,"Ndugu yangu, pole sana ikiwa umekuwa unadhani sikujali. Kwa kweli, hata ungeniomba moyo wangu siku hizo ningekupa tu. Unajua tena sisi Nyani, Tumbili na Kima tuna mioyo mingi. Hata hivyo, nasikitika kuwa Mungu alituambia kuwa daima mioyo yetu itakaa mitini. Basi ndugu mpenzi, badala ya kuendelea na safari hii, turudi pale mtini nikupe moyo wangu pamoja na mitatu ya wanangu kusudi uwalishe wanao na mkeo."

Mamba akaingia mtegoni. Wakarudi hadi ufuoni. Kwa vile Mamba hakuweza kutoka majini, alibaki ufuoni akimngojea rafiki yake amletee mioyo.

Mamba alitunga macho yake kwenye ujia alioufuata Nyani akiomba pasitokee lolote la kumchelewesha Nyani. Matumbo yalimnguruma kwa njaa. Roho ikampapa kwa tumaini. Alingoja, akongoja, akangoja... wiki, mwezi, mwaka... Nyani hakurudi. Mamba akajua amepwaguliwa na Nyani. Akaapa kumtafuta kwa udi na ambari. Huo ukawa mwisho wa urafiki kati ya Nyani na Mamba. ***Hadithi yangu inaishia hapo.***

**Maswali**

k) Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha.
(alama 2)

l) Tambua mbinu **sita** kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu.
(alama 6)

m) Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo **matano** muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako.
(alama 5)

n) Fafanua umuhimu wa ngano hii katika jamii.
(alama 3)

o) Kwa kutoa hoja **nne** jadili umuhimu wa maneno yaliyokolezwa rangi katika utambaji wa ngano kama hizi.
(alama 4)

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………

......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................
......................................................................................................................

KWA MAJIBU PIGA SIMU KWA MWALIMU ABRAHAM **0729125181**

**JINA ……………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA…………………**

**SHULE………………………………….. ……SAHIHI…….………..……………………..**

**TAREHE…………………..……………LENGO…………….……………………………….**

**102/3**

**KISWAHILI.**

**KARATASI 3**

# SERIES 5 KCSE MOCK

**FASIHI**

**MUDA: SAA 2 1/2**

*Hati Ya Kuhitimu Elimu Ya Sekondari*

**KISWAHILI KARATASI YA 3**

**KIDATO CHA NNE**

**Maagizo**

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

(c) *Jibu maswali manne pekee.*

(d) *Swali la **kwanza** ni la lazima.*

(e) *Kila swali lina alama ishirini (20)*

(f) *Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki: yaani; Ushairi, Tamthilia , Hadithi fupi na Riwaya.*

(g) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

(h) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa*

*sawasawa na kuwa maswali yote yamo*

**SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI**

**Swali Ia Iazima**

1. (a) Tofautisha kati ya mighani na maghani. (alama 2)

(b) Taja na ueleze ama tatu ya maghani ya kawaida. (alama 6)

(c) Eleza sifa za maghani. (alama 4)

(d). Kwa kurejelea mifano mwafaka eleza majukumu manane ya nyimbo katika jamii, (alama 8)

**SEHEMU B: USHAIRI**

***Jibu swali la 2 au la 3***

**2.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***.

Ewe hisia!
Umeniamshia ndoto niloisahau zamani
nyimbo ya kale
na mdundo usonivutia
ila hayawani na mwangu rohoni.

Tulia sasa tulia
Hebu tulia ewe hisia ulo mtimani
Nataka katu kusisimka
kwa sauti yako laini
Kwani njia zetu ni
daima hazioani

Umesubutu vipi kuniita
    kutoka mwako ngomeni
    ulimosahauliwa tangu zamani
Basi yawache maombolezi yako yaso maoni,
    yawateke hao mashujaa wa kale
    wafu walo kaburini.

Hebu tulia, usiniingilie
    Usinihangaishe!
Kukuandama katu haimkini
Kwani hata sasa…kwa kukuwaza tu dakika hini
    naona majuto ya mbali moyoni
    kama kwamba nimegawa wangu wakati
    na wazimu, majinuni.
Basi nenda zako hisia…shuu…hebu tokomea.

**Maswali**

(a) Huu ni utungo wa aina gani? (alama 2)

(b) Huku ukitoa mifano, fafanua sifa zinazoufanya utungo huu kuwa shairi (alama 5)

(c) Mistari mishata ni nini? Toa mifano kwenye shairi hili. (alama 4)

(d) Fafanua tamathali za kifasihi katika shairi hili. (alama 3)

(e) Eleza mbinu **tatu** alizotumia mtunzi kutosheleza kaida za kishairi. (alama 6)

**3.** ***Soma shairi lifwatalo kisha uyajibu maswali yanayoliandama:***

Naandika yangu haya, kwa uwezo wa Wadudi,
Kanipa njema afiya, kumsifu sina budi,
Nifundishie insiya, hino methali ya jadi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo

Ago mchama huuya, mbele mambo yakizidi,
Hurudi pakawa kaya, kupapenda hana budi,
Kwingi angawayawaya, ago shuruti arudi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Kule kwetu Mwarakaya, kijiji chetu cha jadi,
Yalidhihirika haya, bwana mmmoja mkaidi,
Aloalikwa ulaya, kadhani 'mepata sudi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo,

Alidhani hatauya, 'endapo nchi ***baidi***,
Na kusema bila haya, kwa inda na ukaidi,
Kwamba akenda ulaya, harudi kwenya samadi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Aliranda akitaya, kwa mbwembwe na zake tadi,
Nguo moto kazitiya, nyumbaye akainadi,
Kasema vyote 'ishiya; kurudi sina ahadi
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Matusi aliyamwaya, mengi yasiyo idadi,
Mkewe kamwita yaya, na kudharau abidi,
Kanena ***'mekata waya'***, ng'ambo nenda kufaidi,
Mchama ago hayeli, huenda akauya papo,

Ng'ambo alielekeya, kwa vishindo kama radi,
Kumbe aliyemwendeya, kabambwa kwa ufisadi,
Vya watu amebugiya, rushwa na kuhepa kodi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo.

Kombo yakamwendeya, mambo mno yakazidi,
Akabakia kuliya, nyumbani ataka rudi,
Nyumba ipi 'taingiya', hana tena tabaradi,
Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo

***Maswali***

a) Kwa kutolea ushahidi ufaao shairini, jadili kifupi maswala **matatu** makuu ambayo mtunzi ameyashughulikia. (alama 6)
b) "Mtunzi huyu ni bingwa wa kutumia lugha kupitisha ujumbe." Tetea. (alama 4)
c) Fasiri ujumbe wa mtunzi katika ubeti wa **sita**. (alama 4)
d) Nafsi nenewa katika shairi hili ni nani? Thibitisha. (alama 2)
e) Zaidi ya tarbia, ungelipangaje tena shairi hili? (alama 2)
f) Fafanua msamiati ufwatao kama ulivyotumika shairini: (alama 2)
    a) Baidi

b) ‘mekata waya’

**SEHEMU C: TAMTHILIA*: BEMBEA YA MAISHA (Timothy Arege* )**

**Jibu swali la 4 au 5**

4.”Basi usijipandishe presha bure mama!”

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)

(b) Ainisha mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwakatika dondoo hili. (alama2)

(c)Eleza sifa za msemewa. (alama 4)

(d) Jadili maudhui ya utamaduni kama yanavyojitokeza katika tamthilia nzima.

(alama10)

5. Katika tamthilia hii Maisha yamesawiriwa kama Bembea. Kwa kutolea mifano mwafaka oanisha kauli hii na wahusika mbalimbali. (alama 20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI : MAPAMBAZUKO YA MACHWEO (*D.W Lutomia na Phibbia Muthama)***

**Jibu swali la 6 au 7**

6...iwapo penzi hili litatia doa,basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya

kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake..."

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b)Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. (alama 4)

c)Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)

d)Eleza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. (alama 6)

7. Swala la elimu limepewa kipaumbele katika hadithi ya Sabina. Jadili (alama 20)

**SEHEMU E: RIWAYA CHOZI LA HERI : Assumpta Matei**

**Jibu swali la 8 au 9**

8.Eleza jinsi **maudhui ya ufisadi** yalivyoshughulikiwa katika riwaya ya Chozi la Heri.

(alama 20)

*9*."…liandikwalo ndilo liwalo? Since when has man ever changed his destiny?"

15. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
16. Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 6)
17. Kwa kuzingatia hoja **kumi**, jadili jinsi ambavyo hali ya, **" liandikwalo ndilo liwalo''**, inavyojitokeza katika Chozi la Heri. (alama 10)

**JINA …………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA…………………**

**SHULE……………………………………..……SAHIHI……..……..……………………..**

**TAREHE…………………...……………LENGO…………….……………………………….**

**KIDATO CHA NNE**

**KISWAHILI 102/3**

# SERIES 6 KCSE MOCK

**SEHEMU YA A**

**Swali la lazima**

**(vii) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo;**

Sinisumbue akili, nakusihie mwandani,
Afiya yangu ni dhalili, muno nataka amani,
Nawe umenikabili, nenende sipitalini,
Sisi tokea azali, twenda zetu mizimuni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani,
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini,
Kwa nguvu ya kirijali, mkuyati uamini,
Kaafuri pia kali, na dawa ya ndwele fulani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini,
Dawa yake ni shubili, au zogo huauni,
Zabadi pia zahali, kwa maradhi yako ndani,
Au kwenda wasahili, wenyewe walo pangani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini,
Daktari kuona mwili, tanena kansa tumboni,
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni,

Ukatwe kama figili, tumbo nyangwe na maini,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Japo maradhi dhalili, kuteguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana Kifani,
Waambiwa damu kalili, ndugu msaidieni,
Watu wakitamali, kumbe ndio buriani,
Nifuateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

Mizimu yakupa kweli, wakueleze undani,
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu dhamani,
Ulete kuku wawili, wa manjano  wa kijani,
Matunda pia asali, vitu vya chanoni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani!

**Maswali**

c) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 2)
d) Liweke shairi hili katika bahari mbili. (alama 2)
e) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
f) Kwa nini mshairi anakataa kwenda hospitali? (alama 2)
g) Ni nani nafsi neni katika shairi hili? (alama 1)
h) Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)
i) Eleza muundo wa ubeti wa pili. (alama 4)
j) Eleza jinsi uhuru wa  kishairi ulivyotumika katika shairi hili. (alama 2)
k) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
   15.Pangani
   16.Nenende

**SEHEMU YA B: HADITHI FUPI: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE.**

(viii) "Yu wapi kirukanjia wako? Wajua yuko wapi? Uliacha mbachao kwa msala upitao. Atakutunza nani, maana kwako fadhila za punda ni mashuzi!"

(viii) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

(ix) Taja mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 2)

(x) Bainisha toni ya dondoo. (alama 1)

(xi) Fafanua sifa zozote tatu za mzungumziwa. (alama 3)

(xii) Kwa kurejelea hadithi "Fadhila za punda" onyesha ukweli wa kauli kuwa fadhila za punda ni mashuzi kwa mifano mwafaka. (alama 10)

**Au**

(ix) Huku ukirejelea hadithi zifuatazo tano jadili maudhui ya migogoro kwa kutoa mifano maridhawa. (alama 20)

18. Fadhila za punda
19. Msiba wa kujitakia
20. Mapambazuko ya machweo
21. Harubu ya maisha

**SEHEMU YA C: RIWAYA YA CHOZI LA HERI**

(x) "Kisa cha kaniki cha usiku wa manane kimetanda. Anayetazama anamwona mja aliyevaa koti kuukuu…..Anaimba huku ameshika chupa mkononi….."

f) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

g) Tambua aina nne za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

h) Fafanua maudhui yanayochangiwa na mrejelewa huku ukirejelea riwaya. (alama 2)

i) Eleza sifa tatu za mrejelewa. (alama 3)

(xi) Changanua kifungu kifuatacho.

(xvi) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. (alama 10)

Mkuu wa shule, walimu na wanafunzi wenzangu, suala la uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu. Tumeona jinsi misitu ilivyovamiwa na viongozi wenye mate ya fisi. Naskia baadhi ya vinara wa taasisi mbalimbali za umma wamewaacha wanyama kama mayatima kwa kupoka makazi yao. Maelfu ya maekari ya misitu yamefyekwa na kujengwa viwanda. Badala ya mibambakofi na miti mingine inayosafisha hewa, michai imetwaa nafasi yake. Wanaohusika na matendo haya wanapoulizwa hudai kuwa michai si adui wa mazingira! Wengine wanasema kuwa misitu haina budi kukatwa ili kupanda mimea inayotoa chakula, kwani jamii sharti ijitosheleze kwa chakula.

(xvii) Mbali na maswara yanayojitokeza katika kifungu, eleza namna mwandishi alivyoshughulikia uharibifu wa mazingira katika riwaya ya chozi la heri. (alama 6)

(xviii) Jadili mchango wa vijana katika kubomoa jamii katika riwaya ya chozi la heri. (alama 4)

## (xii) <u>SEHEMU YA D: TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA</u>

"Mwanangu binadamu mchoyo kwa lake lakini mkarimu ajabu kwa la mwenziwe. Atakukarimu kwa la mwenziwe na atakupa nyongeza usiohitaji lakini lake atalizika katika giza la kina cha moyo wake. Ndiyo hulka yake mwana wa Adamu."

a. Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
b. Jadili namna chanya msemaji na wenzake wa jinsia ya kike walivyosawiriwa katika tamthilia ya Bembea ya maisha. (alama 6)
c. Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya msemaji na msemewa katika tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama 10)

(xiii) Jadili maudhui yafuatayo kwa kutolea mifano maridhawa kama yanavyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea ya maisha.

13. Mabadiliko
14. Migogoro

## (xiv) <u>SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI</u>

Dunia hii ina matatizo x2
Watu wengi hawajajua
Ni dunia yataabu
Hata hivyo usijali.

Karibu malaika karibu x2
Mimi nikukaribishe
Kwa mikono yote miwili
Dunia mti mkavu.

Usilie mtoto usilie x2
Kwa kuiona dunia
Iliyo na masumbuko
Umebebwa miezi tisa.

**Maswali**

3. Huu ni wimbo wa aina gani? (alama 1)
4. Eleza ujumbe wa wimbo huu. (alama 2)
5. Eleza sifa za nyimbo za bembea . (alama 4)
6. Taja tanzu kuu nne za fasihi simulizi. (alama 4)

j) Unanuia kukusanya data za kipera kilicho hapo juu. Pendekeza njia tano utakazotumia. (alama 5)

k) Eleza changamoto nne utakazokumbana nazo katika kukusanya data zako. (alama 4)

JINA ……………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA…………………

SHULE………………………………………..……SAHIHI……..………..………………………..

TAREHE…………………...…………LENGO…………….…………………………………

**KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION**

**102/3 KARATASI YA 3**

**KISWAHILI.**

**FASIHI**

# SERIES 7 KCSE MOCK

**TIME :2.30 hrs**

**Maagizo**

l) Andika jina lako kwa nafasi ulioachiwa hapo juu

m) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu

n) Jibu maswali manne pekee

**o)** Swali la **kwanza** ni la **lazima.**

**p)** Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu zilizobaki (**hadithi fupi,tamthilia riwaya na fasihi simulizi)**

q) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | JUMLA | |

SEHEMU A:**USHAIRI**

**LAZIMA .1**

Naikumbuka ,

siku nilipofika kijijini

na kumkuta nyanya kaketi chini ya,

mgunga unaolekeana na machweo,

akisaga ugoro wake

na

kuyaangalia machweo,

akiwasikiliza nyuni waliokuwa,

wakiimba kwa msisimko

kuyaomboleza matanga ya

magharibi.

Naikumbuka kauli yake,

‘itakuwa lini nasi kuomboleza

Kifo cha dhiki?

Naikumbuka sauti ya

mama alipokuwa akiwinga

bundi aliyekuwa akiimba

mbolezi kuucheka umaskini

kuudhihaki uwezo duni wa wanakijiji.

Naikumbuka sauti ya mama

Na swali lake:

‘Lini nasi tutawaimbia watutesao

mbolezi za bundi?

Naikumbuka siku niliposikika,
kilio alichokilia ndugu;
kidole ki lipokatwa na mashine
ya kutengenezea karatasi
Sauti yake akilalamika,
kutolipwa fidia na chozi,
la kufutwa kazi kwa kutozalisha,kama kabla.
Ndio na swali lake:
'Lini itakatwa mirija ya
wanyonyaji wafanyao watu mashine?

Naukumbuka ukwenzi,
alioupiga falahi na mkulima,
aliyepokea pesa ukufi kwa,
mazao yaliyomlaza nje na kumvunja,
mgongo akalala hoi,
nayakumbuka machozi yake ,
yaliyotiririka na kumkamua
nguvu akitoa lawama zilizotoka kwa shida
nililisikia swali lake:
'Lini jasho la upanzi na mavuno
litawafaidi wachomwa na jua?'

(xix) ‘’Shairi hili linakatisha tamaa.’’ Thibitisha kauli hii kwa mifano mitatu kutoka kwenye shairi. (**alama 3**)

(xx) Fafanua umuhimu wa aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili.(**alama 2**)

(xxi) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (**alama 2**)

(xxii) Jadili umuhimu wa maswali ya balagha katika shairi hili. (**alama 2**)

(xxiii) Tambua toni ya shairi hili. (**alama 1**)

(xxiv) Bainisha na uoneshe umuhimu wa mistari ifuatayo katika shairi hili.

17. Mistari kifu (**alama 2**)
18. Mistari mishata (**alama 2**)

(xxv) Bainisha aina mbili za taswira zinazojitokeza katika shairi hili. (**alama 2**)

(xxvi) Fafanua muundo wa shairi hili . (**alama 4**)

SEHEMU YA .B **HADITHI FUPI**

**Jibu swali la 2 au 3**

**15. D.W .LUTOMIA : *Msiba wa kujitakia***

**Wetu ni wetu ,hata akiwa mbaya …ni wetu.hatuna budi kuchagua yeye .lisilobudi hubidi.**

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4)**

(b)Fafanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hii. (**alama 4**)

(c)Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai.jadili.(**alama 12**)

AU

3.**YUSSUF SHOKA HAMAD** :***Mzimu wa Kipwerere***

**“Mbali na vitisho vya aina hii,mzimu wa kipwerere ulikuwa na miiko yake”**

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4**)

(b) Fafanua sifa za msemaji wa maneno haya. (**alama 4**)

(c)Jadili miiko ya mzimu wa kipwerere kwa mujibu wa hadithi. (**alama 4)**

(d) Dondoa vitisho vinavyorejelewa kwa mujibu wa hadithi. (**alama 8**)

SEHEMU YA .C. **BEMBEA YA MAISHA (Timothy M.Arege)**

**Jibu swali la 4 au 5**

(**4)"Lakini nilivyosema ,mungu hamwachi mja wake.."**

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4**)

(b) Tambua sifa tatu za msemewa. (**alama 3**)

(c)Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kukuza vipengele vifuatavyo.

(i) Ploti (**alama 4** )

(ii) Maudhui (**alama 4**)

(d) Kwa kurejelea tamthilia nzima eleza ukweli wa kauli "mungu hamwachi mja wake".(**alama 5**)

**AU**

(**5**) **Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli.Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema .amri na vitisho kama askari.Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa.Katika wodi hewa iliyojaaa harufu ya dawa imezagaa,vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura.Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.matumaini yanadidimia .Tumaini lako unaliweka katika sala.**

(a) Tambua toni mbili katika kifungu hiki (**alama 2**)

(b) Tambua aina moja ya taswira katika dondoo hili (**alama 2**)

(c)Kando na taswira chambua vipengele vingine vya kimtindo (**alama 6)**

(d) Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia kujenga tamthilia ya bembea ya maisha (**alama 10)**

SEHEMU YA .D

**CHOZI LA HERI (Assumpta K.Matei)**
**Jibu swali la 6 au 7**

6.**‘’Amani iwe nanyi.’’**
**‘’Iwe pia nawe.’’**
(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4**)
(b)Onyesha kinyume kinachojotokeza katika kauli iliyopigiwa mstari kwa kuwarejelea wanaolengwa na maneno haya. (**alama 16)**

**AU**

7.**‘’Wanawake ni viumbe wa kushangaza sana.Ya nini kuilea mimba kisha kuja kutupa matokeo ?’’**

g) Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4**)
h) Eleza umuhimu wa anayeambiwa maneno haya kuijenga riwaya hii. (**alama 4**)
i) Kwa kurejelea riwaya hii ,onyesha mchango wa wanawake katika kuzoroteka kwa Maisha yao (**alama 12**)

SEHEMU YA .E

**FASIHI SIMULIZI**

Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali

Heri ujue mapema

Nasaba yetu haina woga

Woga haumei kwetu,humea kwa kina mamaku.
Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah!kisu cha ngariba ni kikali ajabu.
Iwapo utatikisa kichwacho.
Uhamie kwa wasotabiri,
Ama tukwite njeku.
Mpwangu kumbuka hili,
Wananume wa mlango wetu
Si waoga kwa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali
Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia

Sema unachotaka

Usije kunitia aibu

**Maswali**

22. Taja na uthibitishe shughuli zozote za jamii ya wimbo huu. (**alama 4**)
23. Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? (**alama 2**)
24. Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha. (**alama 2**)
25. Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume .Thibitisha kauli hii. (**alama 2)**
26. Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii. (**alama 6**)
27. Ijapokuwa nyimbo ni nzuri ,zina ubaya wake.Thibitisha kauli hii . (**alama 4**)

JINA ……………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA………………….

SHULE…………………………………….. ……SAHIHI……..………..………………………..

TAREHE…………………...……………LENGO…………….………………………………….

*Cheti cha Kuhitîmu Kisomo cha Sekondari*

## KIDATO 4, 2023

**SERIES 8 2023 KCSE MOCK**

# 102/3

## KISWAHILI (FASIHI) KARATASI YA 3

Saa: 2'Z2

Series 8 2023 KCSE

28. *Jibu maswali manne pekee.*
29. *Swali la **kwanza** ni la **lazima.***
30. *Maswali hayo mengine matatu yacl*ı*aguliwe kutoka sehemu nne zilizobakî; yaani.Riwaya, Fasihi Simulizi, Tamthilia na Ushairi.*
31. *Usîjibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
32. *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
33. *Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kîjitabu cha majibu ulichopewa.*
34. *Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.*
35. *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*
36. *Andika nambari kwa maswali uliyoyajibu kwenye jedwali ulilochorewa hapo chini.*

| **Swali** | **Upeo** | Alama |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU A: USHAIRI

1. ***Soma shairi lifuatalo Kisha ujibu maswali***

Kama akili si ma1i,maskini na tajiri,
Wangali moja sampu1i, asikuwepo fakiri,
Na hangekuwa na ma1i,mwinyi bila kufikiri,
Kama akili si ma1i,usingeweza fıkiri

Ukeshapo kwa fikara,ni kwa wingi mwa akili,
Kuwaza kigaragara,una mengi si akili,
Na kuwa una tambara,metajirika kwa hili,
Kama akili si mali, usingeweza fıkiri.

Alokijenga kitanda,ana wingi wa akili,
Hata asiwe na bunda,hamithili kwa akili,
Hata naye paka nunda,pasipo akili hali,
Kama akili si mali,usingeweza fıkiri,
Akili kweli ni mali,kwa kuteua vya mwozo,
Singetumia akili,ungevila vya angamizo,
Afya ikawa thaki1i,na kuhiliki mawazo,
Kama akili si ma1i,usingeweza fıkiri,

Vipi gonjwa kikuganda,wawazia sipitali,
Huachi ukawa ng'onda,ukanyauka muwili,
Ugangani unakwenda,kutafla afadhali
Kama akili si ma1i,usingeweza fikiri,

Kama akili si mali,kusingekuwa na jela,
Kuwatenga kuwa mbali,wenye hiana na hila,
Kwa mbavu na ufıdhu1i,pamwe mbinu
tolatola
Kama akili si ma1i,usingeweza fıkiri,

Tajiri na maskini,wote wanayo akili,
Ni kuwa hayafanani,waliyonayo
makali,
Kabisa hawashibana,liwe lile au hili,
Kama akili si ma1i,usingeweza fikiri,

Kama akili si mali, 'singekuwa na hazina,
Ya kudadisi methali,na kupinga yako mama,
Gani inadumu ma1i,ku1iko huko kusana?

Kama akili si mali,usingeweza fikiri.

**Maswali**

16. Eleza dhamira ya mshairi (alama 2)
17. Andika mifano ya vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili (alama 4) i. Sitiari

ii. Tanakuzi iii.
Swali la balagha iv.
kinaya

c) Tambua na ueleze nafsi neni katika shairi hili (alama 2)
d) Eleza toni ya shairi hili (alama l)
e) Onyesha jinsi idhini ya mshairi ilivyofanikiwa (alama 4)
f) Andika umuhimu wa aina mbili za urudiaji zinazojitokeza katika shairi hili (alama 4)
g) Bainisha bahari ya shairi hili (alama 3)

**SEHEMU B: BEMBEA YA MAISilA-Timothy Arege.**

**2.** "Dunia hii ya sasa tunaishi katika hofu.Tunahofu hata tusichokifahamu."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili (alama 2)
c) Fafanua sifa nne za msemaji wa maneno haya. (alama 4)
d) Eleza jinsi hofu imejitokeza katika tamthilia. (alama 10)

**3.** (a) Jadili maudhui yafuatayo kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya Maisha
i. Maradhi/afya (alama5) ii. Nafasi ya mwanamke katika jamii (alama5)

(b) ...leo hii kikapu cha mama kimejaa ndago.

i. Tambua mbinu/tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili

(alama 2) ii. Kwa kurejelea tamthilia nzima,toa mifano ya mbinu uliyoitambua katika (alama 8)

**SEHEMU C:MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE Lutomia na Phabian Muthama.**

j) Kwa kurejelea hadithi **Fadhila** za punda katika mapambazuko ya machweo na hadithi nyingine, Jadili maudhui yafuatayo;
i. Nafasi ya mwanamke katika jamii. (alama 10) ii. Ndoa (alama 10)

k) "Mwanangu, nizike duniani unifunike..."
a. Fafanua muktadha wa maneno hata (alama 4)

b. Taja na utolee mfano mbinu moja ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili (alama 2)

c. Ukirejelea hadithi ya "Mzimu wa kipwerere", Fafanua jinsi Imani katika Mambo ya kichawi yamejikita katika jamii. (alama 14)

**<u>SEHEMU D : CHOZI LA HERI -Assumpta Matei</u>**

r) "Nitapigana kwa jino na ukucha kuulinda utu wangu, Nitatafuta haki ilikojificha."

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b. Kwa kutolea mifano, tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili (alama 4)

c. Eleza umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (alama 4)

d. Eleza toni iliyotumika katika dondoo hili (alama2)

e. Kwa kutolea mifano riwayani, thibitisha namna binadamu alivyopungukiwa na utu. (alama 6)

s) a) Maovu yametamalaki katika jamii ya Riwaya ya Chozi la Heri. Tetea kauli hii kwa kutolea hoja kumi. (alama 10)

b) Fafanua namna mbinu ya sadfa ilivyotumiwa katika Riwaya. (alama 10)

**SEHEMU E:FASIHI SIMULIZI**

**8.** Eleza maana ya istilahi hizi katika Fasihi Simulizi

(i) Tondozi (ii) Pembezi (iii)Hodiya (alama 3)

(i) Mlumbi ni Nani? (alama 1)

(ii) Fafanua sifa tano za mlumbi bora. (alama 5)

Orodhesha hasara sita za miviga. (alama 6)

Fafanua jinsi jamii yako inajaribu kuhifadhi Fasihi Simulizi. (alama 5)

**JINA ……………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA…………………**

**SHULE…………………………………….……SAHIHI……..………..……………………..**

**TAREHE…………………..…………LENGO…………..…………………………………**

102/3

KISWAHILI- fasihi

Karatasi 3

MUDA: SAA 2 ½

# SERIES 9 KCSE MOCK 2023

**MAAGIZO**

1. Jibu maswali manne pekee

2. Andika majibu yako kwa lugha ya Kiswahili.

3. Swali la kwanza ni la lazima

4. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:- Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi

5. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

**Kwa Matumizi Ya Mtahini Pekee**

| SWALI | UPEO | TUZO |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| **Jumla** | 80 | |

**1. SEHEMU A: USHAIRI (LAZIMA)**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata.

**SIKATE TAMAA**

Umeanguka, inuka, simama kama mnazi
Umechunika, inuka, tia dawa kwa ujuzi
sasa inuka, inuka, kijana ianze kazi
Sikate tamaa

Usife tamaa, nyanyuka, ni muweza wa kutenda
Kuna hadaa, nyanyuka, anza tena kujipinda
Dunia baa, nyanyuka, anza tena kujiunda
Sikate tamaa

Sivunjwe moyo, dunia, hivyo itakunyanyasa
Futa kiliyo, dunia, hiyo idhibiti sasa
Ipe kamiyo, dunia, kamwe, siache kufusa
Sikate tamaa

Una nguvu, simama, wewe upambane nao
Una werevu, simama, uzepuke njama zao
Usiche kovu, simama, ujifunze vumilio
Sikate tamaa

a) Hili ni shairi la aina gani? (al. 1)

b)Onyesha mbinu mbili za lugha katika shairi hili.
(al. 4)

c) Eleza muundo wa shairi hili. (al. 4)

d) Tambua idhini ya mshairi.
(al. 3)

e) Eleza maudhui ya utungo huu.
(al. 2)

f) Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. (al. 4)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (al. 2)

i)baa

ii) kovu

**TAMTHILIA: BEMBEA YA MAISHA- TIMOTHY AREGE**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. Ninasikia jiji lina watu wengi, magari mengi, barabara nyingi, majengo makubwamakubwa tena mengi… Wanasema ukiwa mgeni ni kama msafiri jangwani.

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)

b) Kwa kutoa mifano, eleza mbinu za lugha zinazojitokeza hapa. (al. 4)

c) Kwa hoja sita, jadili maovu yanayotokea katika jumuiya ya tamthilia Bembea ya Maisha. (al. 12)

3. Lakini maskini mwanangu hatuonani! Ninamwona tu akiwa usingizini. Sisemi naye, sili naye, sichezi naye… Uzazi gani huu sasa?

a) Weka dondoo hili katka muktadha wake (al. 4)

b) Kwa kutoa mifano, eleza mbinu za lugha zinazopatikana kwenye dondoo hili. (al. 4)

c) Maisha ya mwanadamu yamejaa matatizo. Jadili ukirejelea jumuiya ya Tamthilia ya Bembea ya Maisha. (al. 12)

**RIWAYA: CHOZI LA HERI-ASSUMPTA MATEI**

Jibu swali la nne au la tano.

4. Woga huweza kumtia mtu upofu wa muda! Hatimaye moyo wa shauku uliyashurutisha macho kukisoma kile ambacho kilichosomeka kama ujumbe wa mauti.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

b) Taja na utoe mifano ya mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (al. 4)

c) Fafanua sifa zozote nne za msemaji. (al. 4)

d) Kwa kurejelea riwaya nzima, eleza jinsi tatizo la ukabila/kimbari lilivyoathiri maisha ya wahusika mbalimbali. (al. 8)

5. Hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe. Jadili ukweli wa methali hii kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri.

(al. 20)

**HADITHI FUPI**

**MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

6. Ucha Mungu si kilemba cheupe. Kwa kurejelea hadithi ya Fadhila za Punda, jadili ukweli wa kauli hii. (al. 20)

**7. FASIHI SIMULIZI**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Mimi ni mkulima anayesifika
kutoka jimbo hadi jimbo
nishikapo jembe langu
udongo unatetemeka
nipandapo mbegu zangu
huchipuka kwa nguvu za ajabu
mimea yangu kipalilia kwa ustadi usio mfano
wakati wa kuvuna
maghala yangu hufurika
kwa juhudi zangu
mimi ni bingwa wa ukulima
mimi ni shujaa wa ukulima
mimi ndiye mkulima asiye mfano

i)

a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi. (al. 2)

b) Eleza sifa nne za kipera ulichotaja. (al. 4)

c) Taja tamathali mbili za usemi zilizotumika katika kifungu hiki. (al. 4)

ii)

a) Miviga ni nini? (al. 2)

b) Eleza dhima ya miviga. (al. 4)

c) Eleza hasara za miviga. (al. 4)

**JINA ………………………………………………...NAMBARI YA MTAHINIWA…………………**

**SHULE……………………………….……SAHIHI…….………..………………………..**

**TAREHE…………………...……………LENGO……………..……………………………….**

**KARATASI YA TATU (102/3)**

**MUDA: SAA 2 ½**

**SERIES 10 2023 KCSE MOCK**

**MAAGIZO;**

t. Swali la kwanza ni la lazima
u. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
v. Jibu jumla ya maswali manne
w. Kila swali ni alama 20
x. Tumia lugha ya Kiswahili

**SEHEMU YA A:USHAIRI (ALAMA 20)**

**Swali la lazima**

**Soma shairi kisha ujibu maswali**

Angawa mdogo dagaa, amekomaa

Kaanga kidogo, atakufaa

Kalia kinaya, h'ondoa njaa

Wa kwako udogo, kijana sio balaa

Na sio mzigo ,kijana bado wafaa

Toka kwa mtego ,kijana sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana ukubwa jaa

Jikaze kimbogo, kijana wacha kukaa

Chimbua mhogo, kijana usibung'aa

Na wake udogo, dagaa hajambaa

Kuliko vigogo ,dagaa hajambaa

Hapati kipigo ,dagaa hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa

Sihofu magego. Kijana nawe wafaa

Kazana kidogo, kijana kugagaa

Maswali

a)Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 2)

b)Eleza arudhi zilizofuatwa katika shairi hili (alama 4)

c)Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake. (alama 3)

d)Tambua bahari katik shairi hili kwa kutegemea;

i)Vipande vya msihororo

ii)Mpangilio wa vina

iii)Idadi ya mishororo (alama 3)

e)Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 3)

f)Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi.(alama 3)

g)Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

**<u>SEHEMU YA B: Riwaya ya Chozi la heri na Asumpta Matei</u>**

2. Athari ya vita katika nchi ya Wahafidhina ni kioo cha bara ya Afrika. Jadili(alama 20)

AU

3. Riwaya ya Chozi la heri imejaa aina mbalimabli za migogoro.Jadili(alama 20)

**<u>SEHEMU YA C: Hadithi ya Mapambazuko na machweo na hadithi nyingine</u>**

4.”Ondoa wasiwasi mhibaka ,***you are in very safe hands*** .Usiulize maswali , its okay. Tulikuja sote jana baada ya ***dance*** , umesahau hivi?’

i) Fafanua muktadha wa dondoo hili.(alama 4)

ii) Taja na ueleze mbinu za lugha zinazojitokeza katika dondoo.(alama 4)

iii) Jadili madhara ya pombe katika jamii kama inavyodhihirika katika hadithi ya Kila mchezea wembe.(alama 12)

Au

5. Eleza matatizo yanayomkumba mtoto wa kike kwa mujibu wa hadithi ya Sabina.(alama 20)

**SEHEMU YA YA D: <u>Tamthilia ya Bembea ya maisha na Timothy Arege</u>**

6. Tambua nafasi ya mwanamke jinsi alivyoshughlikiwa na mwandishi katika Tamthilia hii..(alama 20)

AU

7. 'Ulimwengu umeendelea sana"

a)Weka dondoo katika muktadha wake. (alama 4)

b) Fafanua sifa sita za msemaji.(alama 6)

c)Eleza kwa nini huku kwa msemaji hakujaendelea.(alama 10)

**SEHAMUA YA E: Fasihi simulizi**

8.a)Taja na ufafanue hatua zozote nne za utafiti nyanjani kwa mfuatano wake.(alama 8)

b)Tambua baadhi ya changamoto ambazo mtafiti anaweza kumbana nazo akiwa nyanjani(alama 8)

c) Data iliyohifadhiwa kwa njia ya maandishi inafisha vipi uhalisia wa Fasihi simulizi?(alama 4)

***Mwisho***